**FURSA ZA UWEKEZAJI NDANI YA HALMASHAURI YA MERU**

## 1.0. UTANGULIZI

### 1.1 Jiografia

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ipo Mashariki mwa mkoa wa Arusha na imelala kati ya latitudi $36^{o}5$ na Longitudi $37^{o}5$. Halmashauri ya Meru inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Siha (Kilimanjaro) kwa upande wa kaskazini na mashariki. Kwa upande wa Magharibi inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Kusini inapakana na wilaya ya Simanjiro.

### 1.2 Idadi ya wakazi

Halmashauri ya Meru ina jumla ya wakazi 268,144 kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwezi Agosti 2012. Kati ya wakazi hao wanawake ni 136,880 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 131,264 sawa na asilimia 49.

### 1.3 Utawala

Halmashauri ya wilaya ya Meru ki-utawala inazo Tarafa 3 (Poli, Mbuguni, King'ori), kata 17, vijiji 71 na vitongoji 281 (Angalia Kiambatanisho) na Jimbo moja la Uchaguzi la Arumeru Mashariki.

Vile vile Halmashauri ya Meru inalea Mamlaka ya Mji Mdogo wa Usa River iliyoanzishwa tarehe 01 Januari 2009 kwa kwa mujibu wa kifungu cha 16 na cha 17 cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za wilaya) ya mwaka 1982.

### 1.4 Pato la mkazi (Per Capita Income)

Pato la mkazi kwa mwaka katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa mujibu wa zoezi lililofanywa na Ofisi ya Takwimu Taifa mwaka wa fedha 2009 ni Tshs. 950,000/= ukilinganisha na wastani wa pato la Tshs. 860,000/= katika mkoa wa Arusha na pia ukilinganisha na Pato la Mtanzania kwa ujumla la wastani wa Tshs. 870,000/= kwa mwaka.

### 1.5 Jiografia

Halmashauri ya Meru ina Kanda za Kijiografia kama ifuatavyo:

### 1.5.1 Ukanda wa Juu

Ukanda wa juu upo katika mwinuko wa mita 1,350 hadi 1,800 toka usawa wa bahari, ukanda huu hupata mvua za wastani wa milimita 1,000 kwa mwaka. Ukanda huu unafaa zaidi kwa kilimo cha mazao ya kahawa, mahindi, maharagwe, migomba, mboga mboga na viazi mviringo. Aidha unafaa pia kwa ufugaji wa ndani (zero grazing) kutokana na ufinyu wa eneo la malisho.

### 1.5.2 Ukanda wa kati

Ukanda huu upo katika mwinuko wa mita 1,000 hadi 1,350 toka usawa wa bahari. Ukanda huu hupata mvua za wastani wa milimita 500 kwa mwaka. Mazao yanayofaa kulimwa katika ukanda huu ni pamoja na viazi vitamu migomba, mahindi, mbogamboga, maharage na kilimo cha maua. Pia kuna ufugaji wa ng'ombe wa ndani (zero grazing) na huria kidogo.

### 1.5.3 Ukanda wa chini

Ukanda huu upo katika mwinuko wa kuanzia mita 800 hadi mita 1,000 toka usawa wa bahari na unapata mvua za wastani wa milimita 300 kwa mwaka. Ukanda huu unafaa zaidi kwa kilimo cha umwagiliaji kutokana na vyanzo vya maji kutoka ukanda wa juu. Mazao yanayolimwa kwa kilimo cha umwagiliaji ni mahindi, maharage, migomba, mbogamboga na mpunga. Ukanda huu pia unafaa kwa uchungaji huria wa ng'ombe wa asili na kidogo ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa utaratibu wa zero grazing.

## 1.6 Ardhi

Halmashauri ya Meru ina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba zipatazo 1,268.2 lillilotengwa kwa matumizi kama ifuatavyo:-

- Eneo linalofaa kwa kilimo ni Hekta 81,400
- Eneo linalolimwa ni Hekta 67,931,
- Eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni Hekta 18,745
- Eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji ni Hekta 11,132,

- Eneo la malisho ya mifugo ni Hekta 10,591

- Eneo la maji ni Hekta 570
- Eneo la misitu ya asili ni Hekta 16,371
- Eneo la misitu ya kupandwa ni Hekta 3000
- Eneo la mbuga za wanyama ni Hekta 20,371

## 1.7 Elimu

### 1.7.1 Elimu Msingi na Sekondari

Meru ina jumla ya shule za msingi 113 za serikali na 23 zisizo za Serikali. Vilevile Meru kuna jumla ya shule za Sekondari 54 kati hizo 29 ni za Serikali na 25 zisizo za Serikali. Kwa upande wa taaluma shule za msingi zimekuwa zikifaulisha mwaka hadi mwaka. Mfano mwaka 2010 wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza ilikuwa asilimia 98, mwaka 2011 ilikuwa asilimia 94% na mwaka 2012 ilikuwa asilimia 91.

### 1.7.2Taasisi za elimu zilizopo Ndani ya Halmashauri ya Meru

Taasisi za elimu ambazo ziko Ndani ya eneo la Halmashauri ya Meru ni kama ifuatavyo:

a) Chuo Kikuu cha Makumira;
b) Chuo Kikuu cha Arusha;
c) Chuo cha Nelson Mandela;
d) Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru;
e) Chuo cha Mifugo Tengeru Tengeru;
f) Kituo cha mafunzo ya Uongozi na Maendeleo (formerly Danish Centre)

## 1.8 Mtandao wa Barabara

Meru ina mtandao wa jumla ya kilomita 805.8 zinazofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ambao umegawanyika kama ifuatavyo:

a) Barabara kuu (Lami) Kilomita 48.3
b) Barabara za Mkoa kilomita 87.7
c) Barabara za Wilaya kilomita 248.9
d) Barabara za Vijiji kilomita 420.9

## 1.9 Sekta ya Afya

Meru ina jumla ya Hospitali mbili (Serikali, Shirika la Dini), Vituo vya afya 8 (serikali 6 na viwili ya mashirika ya Dini) na jumla ya Zahanati 47 (Serikali 26, Watu Binafsi 10, Mashirika ya Dini 8 na 3 zinamilikiwa na Mashirika ya Serikali).

# 2.0 HALI YA UCHUMI

Uchumi wa wakazi wengi wa Halmashauri ya Meru hutegemea kilimo, ufugaji, utalii, biashara kubwa, za kati na ndogo.

Sekta ya Kilimo huchangia asilimia 85 ya pato la Wilaya lakini shuughuli za kilimo zimekuwa zikiathiriwa na ukame wa mara kwa mara hasa katika ukanda wa chini ambao hupata mvua mm 500 hadi 800. Katika kukabiliana na hali hii Halmashauri inahimiza kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga skimu za umwagiliaji za ukubwa mbalimbali. Jitihada hizi zimechangia kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa Meru.

## 2.1 Ufugaji Nyuki

Meru ina jumla ya mizinga ya kienyeji 2,226 ambayo huzalisha wastani wa lita 3 na jumla ya mizinga 880 ya kisasa ambayo huzalisha wastani wa lita 10 kwa mwaka.
Mizinga hii inamilikiwa na watu binafsi na vikundi vya wafugaji nyuki katika kata za Songoro, Nkoaranga, Ngarenanyuki, maji ya chai, Nkoanrua, Leguruki, Kikatiti.

## 2.2 Kilimo

### 2.2.1. Eneo la kilimo.

Eneo linalofaa kwa kilimo katika Halmashauri ni hekta 81,400. Eneo linalolimwa ni hekta 67,931 sawa na asilimia 84 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo. Mazao yanayostawi ni pamoja na; Mahindi, Migomba, Kahawa, Maharage, Maua, Mbogamboga, Matunda ya aina mbalimbali.

### 2.2.2 Malengo ya Kilimo

Kwa msimu wa 2012/2013 malengo ya uzalishaji wa mazao ya Chakula na Biashara ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

| NA | LENGO | | |
|---|---|---|---|
| | **ZAO** | **ENEO (HA)** | **UZALISHAJI (TANI)** |
| 1. | Kahawa | 4,922 | 5,648 |
| 2. | Mgomba | 6,760 | 49,345 |
| 3. | Mihogo | 556 | 4,614 |
| 4. | Mahindi | 34,605 | 128,801 |
| 5. | Mpunga | 1,000 | 5,000 |
| 6. | Mbaazi | 7,500 | 7,500 |
| 7. | Ulezi | 137 | 226 |
| 8. | Mtama | 130 | 559 |
| 9. | Nyanya | 670 | 3,350 |
| 10. | Kabeji | 200 | 4,910 |
| 11. | Karoti | 135 | 1,632 |
| 12. | Viazi Vitamu | 160 | 1,160 |
| 13. | Viazi Mviringo | 100 | 935 |
| 14. | French beans | 375 | 1,980 |
| 15. | Parachichi | 136 | 2,329 |
| 16. | Papai | 169 | 4,609 |
| 17. | Vitunguu | 120 | 576 |
| 18. | Alizeti | 4,325 | 10,812 |
| 19. | Maharage | 8,000 | 12,574 |
| 20. | Pilipili hoho | 90 | 135 |
| 21. | Bilinganya | 50 | 75 |
| 22. | Tikiti maji | 112 | 337 |
| 23. | Matango | 10 | 20 |

### 2.2.3 Matumizi ya Pembejeo za kilimo

Meru ni miongoni mwa Halmashauri ambazo wakulima wake wana uelewa mkubwa juu ya matumizi ya pembejeo bora za kilimo. Pembejeo muhimu zinazotumiwa na wakulima ni pamoja na mbolea za kupandia na kukuzia, mbegu na viuatilifu. Pembejeo hizi zinapatikana katika maduka ya pembejeo yaliyopo ndani ya Halmashauri. Kwa sasa maduka ya pembejeo yako 51.

Wastani wa matumizi ya Pembejeo ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini;

**Wastani wa mahitaji na matumizi halisi ya pembejeo muhimu za Kilimo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru.**

| **Aina ya Pembejeo** | **Mahitaji kwa Msimu (Kilo kwa hekta 1)** | **Matumizi halisi (Kilo kwa hekta 1)** |
|---|---|---|
| Mbolea ya Kupandia | 8,491 | 7,200 |
| Mbolea ya kukuzia | 16.200 | 9,600 |
| Mbegu | 420 | 400 |

Halmashauri ya Meru pia ni mnufaika wa mpango wa pembejeo zenye ruzuku ya serikali ambazo zinatolewa kwa mfumo wa vocha.

Mpango wa Halmashauri ni kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora na mbolea kwa Uhakika na kwa wakati. Katika kutekeleza hili, mambo yafuatayo yanazingatiwa;

a) Kuwa na mpango madhubuti wa uzalishaji wa mbegu za mahindi za daraja la kuazimiwa (QDS) katika kata 11 za ukanda wa kati na chini ambako mahindi hulimwa kwa wingi. Kwa sasa kata zenye uzalishaji wa mbegu hizi ni Maroroni, Mbuguni, Leguruki na King'ori;
b) Kuratibu zoezi la utoaji wa pembejeo zenye ruzuku ya serikali kwa Wakulima kwa kusimamia utendaji kazi wa Mawakala, Viongozi wa vijiji na kamati za vocha ili kuhakikisha kuwa mgao unafanyika kwa haki na kunakuwepo tija;
c) Kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na kuhamasisha wakulima kuzitumia ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na Biashara.

### 2.2.4 Matumizi ya Zana bora za Kilimo:

Halmashauri ina hekta. 25,350 zinazofaa kwa kilimo cha matrekta na wanyamakazi. Zana muhimu zinazotumika ni pamoja na matrekta makubwa, matrekta madogo (power tiller) na wanyama kazi.

Idadi ya zana zilizopo ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

| Aina ya Zana | Zilizopo | Nzima | Mbovu |
|---|---|---|---|
| Matrekta makubwa | 270 | 256 | 14 |
| Matrekta madogo (power tillers) | 23 | 22 | 1 |
| Joizi za wanyamaka | 7,750 | 7,750 | 0 |
| Plau za wanyama kazi | 5,203 | 5,250 | 47 |
| Mikokoteni | 1,539 | 1,530 | 9 |
| Ripper | 160 | 160 | 0 |

### 2.2.5 Miundombinu ya kilimo

#### 2.2.5.1. Skimu za Umwagiliaji:

Zipo skimu 37 za umwagiliaji katika Halmashauri, ambazo zinatumiwa na wakulima wadogo. Skimu hizi zina hadhi tofauti katika ubora kulingana na uboreshaji uliofanyika.

Kwa kipindi cha 2007/2008 hadi 2012/2013, jumla ya mifereji 25 ya asili imefanyiwa ukarabati, ambapo kiasi cha shilingi 1,299,762,550.00 kimetumika. Fedha hizi zilitoka katika vyanzo mbalimbali na utekelezaji umefanyika kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPs), FACF na Hazina.

Mchango wa jamii katika utekelezaji wa miradi hiyo imechangia jumla ya shilingi 134,987,230.00, ambao umetolewa kwa njia ya nguvukazi na fedha taslimu.

Kufuatia ukarabati wa skimu hizi eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 8,100 (2007/08) hadi hekta 12,236 (2012/2013 na uzalishaji wa mazao umeongezeka kutoka tani 0.8 hadi tani 3 kwa hekta kwa msimu.

#### 2.2.5.2. Hali ya Maghala:

Yapo maghala 3 ya kuhifadhia mazao katika Halmashauri ya Meru ambayo kwa ujumla yana uwezo wa kuhifadhi zaidi ya tani 1,300 kwa wakati mmoja. Maghala haya yako katika vijiji vya; King'ori (1), Karangai (1) na Malula (1). Maghala haya yana hali nzuri kufuatia ukarabati uliofanyika kupitia wahisani mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri. Hata hivyo Maghala ya Karangai na Malula bado yanafanyiwa ukarabati na hayajaanza kufanya kazi.

### 2.2.5.3. Masoko ya mazao

Yapo masoko 7 ya wazi, ambayo bidhaa mbalimbali zinauzwa yakiwemo mazao ya chakula. Masoko haya yapo katika vijiji vya Usa River, Patandi (Tengeru), Kikatiti, Ngarenanyuki, King'ori, shambarai Burka na Nguruma. Miundombinu ya masoko si ya kuridhisha kutokana na kutofanyiwa maboresho muhimu.

### 2.2.6 Utekelezaji wa mkakati wa kilimo cha mtama

Zao la Mtama katika Halmashauri ya Meru kwa kawaida huoteshwa kwa kiasi kidogo na wakulima wa ukanda wa chini na kati. Zao hili huoteshwa si kama zao la chakula, bali huoteshwa pembeni mwa mashamba ya mazao mengine kama mahindi, maharage au alizeti kwa ajili ya kukinga hayo mazao dhidi ya wanyama waharibifu (guard rows).
Hata hivyo mwisho wa msimu mtama huvunwa na kuuzwa au kuchanganywa na ulezi kwa ajili ya kutengeneza uji, au unga wake kuchanganywa na unga wa mhogo kwa ajili ya chakula hasa wakati wa upungufu mkubwa wa chakula. Kwa hiyo zao la mtama kama chakula ni dhana mpya kwa wakazi wengi wa Halmashauri.

### Kilimo cha mtama

Kilimo cha mtama kinaendelea kuhamasishwa katika Halmashauri ya Meru ambapo tayari hatua zimeshaanza kama ifuatavyo:

a) Mikutano ya uhamasishaji wa kilimo cha Mtama ilifanyika kwa wenyeviti na watendaji wa serikali za vijiji ambapo jumla ya washiriki walikuwa 444 ambao na waliagizwa kwenda kufanya mikutano ya uhamasishaji katika vijiji vyao;
b) Kufanya zoezi la kuwatambua na kuwaorodhesha wakulima wenye utayari wa kulima Mtama ambao watanufaika na ruzuku ya mbegu ya mtama.

### 2.2.8 Taasisi zilizopo ndani ya Halmashauri ya Meru

a) Arusha National Park (ANAPA);
b) National Artificial Insemination Centre (NAIC)

## 3.0 FURSA NA MPANGO WA UWEKEZAJI

## 3.1. MSITU WA USA SPRING

### 3.1.1 UTANGULIZI

Msitu wa Usa springs ambao pia hujulikana kwa jina la kiasili kama Kibola upo Kaskazini mwa mji wa Usa River takiribani umbali wa kilomita tatu kutoka Mji wa Usa River.

Msitu huu unamilikiwa na Halmashauri ya Meru na una ukubwa wa ekari 21 na umezungukwa na vijiji vitatu vya Nkoanekoli, Sangananu na Kiwawa.

### 3.1.2 Vivutio vya Watalii vilivyopo kwenye Msitu wa Usa Springs

a) Wanyama wadogo wadogo (Blue Monkey, Mbega, Swala), Ndege wa aina mbalimbali, Nyoka (Green Mamba) na Wadudu wa aina mbalimbali;
b) Miti mikubwa ya asili yenye mapango na mandhari nzuri;
c) Chemchem nyingi na vibwawa vidogo vidogo vya maji;
d) Hali nzuri ya hewa inayowafanya wageni wengi wanaoingia kupenda kukaa ndani kwa muda mrefu kupumzika.

Msitu wa Usa springs umezungukwa na hotel nyingi za Kitalii kama vile Ngurdoto Mountain Lodge, Ngurdoto View, Shangazi Hotel, Mbega Lodge, Kiboko Lodge, River Tree na Arumeru River Lodge.

Shughuli za kitalii katika msitu huu zilianza muda mrefu na Watalii wamekuwa wakitembezwa katika msitu huo.

### 3.1.3 Uwekezaji unaotakiwa

a) Kutambua na kuweka njia za asili za kupita za miguu (foot trails);
b) Kuweka vituo/sehemu za kupumzika Wageni wanapokuwa ndani ya msitu;
c) Kutenga eneo ndani au pembeni ya msitu litakalotumika kama Camping Site na sehemu ya kulia chakula (Lunch box);
d) Kujenga toilets/washrooms;
e) Kutoa elimu kwa wananchi wanaozunguka msitu juu ya kuandaa chakula/ kahawa kwa wageni na kutengeneza bidhaa ndogo ndogo kama Shanga, Bangili, Mikanda, Pete, Hereni ambavyo hupendwa na Watalii.

### 3.1.4 Faida itakayopatikana kutokana na uwekezaji katika Msitu huu

a) Mapato ya Halmashauri yataongezeka;
b) Ajira husuani kwa vijana;
c) Mazingira ya msitu yatatunzwa kwa kiwango kikubwa hivyo kuongeza hali nzuri ya hewa pamoja na upatikanaji wa maji kwa mji wa Usa River na pia msitu kuwa chanzo cha mvua.

## 3.2. UFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA

Halmashauri ya Meru ilipata kiasi cha hekta 3,267.61 kutoka iliyokuwa Ranchi ya Taifa ya West Kilimanjaro katika vijiji vya Uwiro (1,298.78ha), Ngabobo (881.95ha), Kisimiri Juu (1,086.88ha). Maeneo hayo yanafaa sana kwa ufugaji wa mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na hata mashamba makubwa ya kuku.

### UBORESHAJI WA ENEO HILI

Uboreshaji wa eneo tajwa utazingatia hali halisi ya eneo, aina ya mifugo inayokusudiwa kutumia eneo na idadi ya mifugo inayoweza kulishwa kwa kuzingatia uwezo wa malisho (carrying capacity).

**Shughuli zifuatazo zinatakiwa kufanywa**

Kuhakiki eneo nzima na kuweka uzio katika mipaka ya eneo

Kurekebisha miundombinu katika eneo hilo ikiwemo josho, vibanio, birika za kunyweshea mifugo, na vibanda vya kujikinga na jua au mvua.

**Kuongeza uwezo wa malisho**

Halmashauri inategemea kuboresha malisho yaliyopo kwa kufanya shughuli zifuatazo

i. Kuondoa aina ya majani ambayo ni sumu na hayana lishe bora kwa mifugo
ii. Kupanda upya maeneo yaliyopoteza uoto wake
iii. Kupanda aina nyingine ya malisho lishe nzuri zaidi
iv. Kuanzisha eneo maalum la malisho kwa ajili ya kujifunza wafugaji (Shamba Darasa)

**Ushirikishwaji jamii katika kuendeleza eneo la malisho**

Halmashauri itaendelea kuwashawishi wananchi katika eneo hilo kushiriki katika mkakati wa kuboresha malisho kwa njia ya kuendesha ufugaji wa aina mbalimbali ya mifugo kwa vikundi, mtu mmoja mmoja kwa makubaliano rasmi na Halmashauri.

Halmashauri itahamasisha vikundi vya wafugaji hasa vijana kutumia malisho hayo kuendesha shughuli za unenepeshaji wa mifugo na kuuza (Ufugaji wa kibishara)

## 3.3. UJENZI WA KITUO CHA BIASHARA (BUSINESS CENTRE)

Halmashauri ya Meru ina eneo la ukubwa wa mita za mraba 25,757 mbele ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru iliyopo Usa River ambalo linafaa kwa ajili ya ujenzi wa maduka (Shopping Malls), Benki, Kumbi za starehe, Hoteli na Ofisi mbalimbali.

Miundombinu ya maji, umeme iko jirani lakini pia eneo hili liko pembeni ya barabara ya lami (Arusha-Moshi).

## 3.4. UJENZI WA ENEO LA MAPUMZIKO (PUBLIC PARK)

Halmashauri ya Meru ina eneo la ukubwa wa mita za mraba 8,443 lililopo mbele ya Ofisi za Makao Makuu ya Halmashauri ambalo linafaa kwa ajili kuanzisha Bustani ya kupumzikia ya wananchi.

Bustani hii inaweza kufanyiwa Landscaping kwa mbele karibu ya barabara ya Lami kuonyesha taswira ya Mlima Meru kama ilivyo kwa eneo la Makao Makuu ya EPZ, Mabibo Jijini Dar Es Salaam.

Nyuma ya mlima huo kunaweza kujengwa chumba cha kuonyesha bidhaa za utamaduni wa Wameru na pia kukawa na Mgahawa kwa ajili ya kuhudumia watu watakaotembelea eneo hilo. Eneo lingine linalobaki linakuwa na viti vya kupumzikia chini ya miti ya asili iliyopo.

Miundombinu ya maji, umeme iko jirani lakini pia eneo hili liko pembeni ya barabara ya lami (Arusha-Moshi).

## 3.5. UJENZI WA KITUO CHA MABASI CHA KISASA (MODERN BUS TERMINAL)

Halmashauri ya Meru ina eneo lenye ukubwa wa ekari 42 pembeni ya barabara kuu ya Arusha-Moshi umbali wa kilomita 11 kutoka katikati ya Jiji la Arusha. Eneo hili linahusisha pia eneo la maegesho ya mabasi madogo ya mjini (Town Buses) na Taxi (cabs).

Lengo la mradi ni kujenga Kituo cha mabasi cha kisasa (Morden Bus Terminal). Eneo hili limezungukwa na ekari nyingine 67 zilizotengwa kwa ajili ya miundombinu mingine kama vile Hoteli, Nyumba za kulala wageni (Guest House), Banks, Car Wash, Garage, Vituo vya mafuta, Zahanati, na Maduka.

Mpango huu wa ujenzi wa kituo kipya cha mabasi unafuatia agizo la Uongozi wa Mkoa wa Arusha kuagiza Halmashauri zijenge Vituo vipya vya mabasi nje ya Jiji la Arusha ili kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji.

Miundombinu ya maji, umeme iko jirani lakini pia eneo hili liko pembeni ya barabara ya lami (Arusha-Moshi).

## 3.6. UJENZI WA KITUO CHA MALORI CHA KISASA

Halamshauri ya Meru imetenga eneo la ekari 25 kwa ajili ya kujenga kituo cha kisasa cha malori makubwa kwa ajili ya kupakia na kushusha mizigo.

Eneo hili litakuwa na miundombinu kama vile garage, car wash, fence na maghala (Warehouses) kwa ajili ya kuhifadhia mizigo. Mradi utakuwa na mitambo ya kisasa ya kupakia na kushusha mizigo.

Lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano unaosababishwa na malori makubwa ya mizigo yanayoingia katikati ya Jiji la Arusha.

Mradi utakapokamilika, malori makubwa ya mizigo hayataruhusiwa tena kuingia katikati ya Jiji. Mizigo itakuwa ikishushwa katika kituo hiki na malori chini ya Tani 10 ndio yatakayoruhusiwa kuingia katikati ya Jiji.

Miundombinu ya maji, umeme iko jirani lakini pia eneo hili liko pembeni ya barabara ya lami (Arusha-Moshi).

## 3.7. UJENZI WA KITUO CHA MICHEZO (SPORTS CENTRE)

Halmashauri ya Meru imetenga eneo la ekari 25 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Michezo cha kisasa katika eneo la Valeska.

Kituo hicho kitakuwa na viwanja vya michezo ya Mpira wa Miguu (Football), Mpira wa Pete (Netball), Mpira wa Kikapu (Basketball), Mpira wa Meza (Table Tennis), Mpira wa Wavu (Volleyball), Ngumi (Boxing), Riadha, Hockey, Squash, Badminton, Golf nk.

Kituo hicho pia kitakuwa na kumbi za kisasa kwa ajili ya mikutano, vyumba vya madarasa, vyumba vya kulala wachezaji. Kituo hiki kikikamilika kinaweza kutumia fursa za timu mbalimbali zinazotaka kuweka kambi mahali penye utulivu na hali ya hewa nzuri kama ya Arusha.

Kituo hiki pia kinaweza kutumika kukuza vipaji kwa michezo mbalimbali kama vile Mpira wa Miguu, Riadha, Ngumi nk.

## 3.8 UANZISHAJI WA ENEO MAALUM KWA AJILI SHUGHULI ZA SPECIAL ECONOMIC ZONE (SEZ)

Ukanda wa uwekezaji Tanzania ni programu iliyoanzishwa mwaka 2005 baada ya kutungwa kwa Sheria ya Ukanda wa uwekezaji ya mwaka 2005.
Sheria nyingine zinazokwenda sambamba na hii ni Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997. Programu hii imekusudia kuvutia uwekezaji katika maeneo maalum/tengefu kwa lengo la kuleta ushindani wa kimataifa ili kukuza uchumi kutokana na kuuza bidhaa katika soko la kimataifa.

Halmashauri ya Meru imetenga eneo la ukubwa wa ekari 4,000 karibu na uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro International Airport (KIA).

Eneo hili litatumika maalum kwa ajili ya shughuli za biashara ambapo kutakuwa na viwanda na Maghala makubwa (Warehouses), Maduka makubwa, ofisi mbalimbali, Hoteli, Kumbi za starehe, nk.

Miundombinu ya maji, umeme iko jirani lakini pia eneo hili linafikika kwa barabara ya lami, ndege na reli (inahitaji kufufuliwa)

### Fursa zinazoweza kupatikana katika ukanda wa uwekezaji

Ili kutosheleza madhumuni yaliyotajwa, Halmashauri ya Wilaya ya Meru imetenga eneo la ekari 4,000 katika kijiji cha Malula, Kata ya King'ori ambazo zitatumika kukuza shughuli za uwekezaji katika sekta binafsi na makampuni ya Kimataifa kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na kutoa huduma mbalimbali.

### Aina ya fursa zinazoweza kuendelezwa

- Uanzishaji wa kiwanda cha kutengeneza chokaa kutokana na kuwepo kwa madini ya "Potash ash" katika eneo la Malula na maeneo mengine ya jirani, uwekezaji katika uzalishaji bidhaa za "gypsum" unaweza kuwa wa manufaa kutokana na kuwepo kwa madini hayo.

- Uanzishaji wa kiwanda cha kusafisha na kutengeneza bidhaa za vito vya thamani. Migodi ya madini ya Mererani itatoa malighafi ya kuwezesha utengenezaji wa bidhaa hizo.
- Kiwanda cha kusindika na kupakia nyama- shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na kienyeji, mbuzi, kondoo n.k zinafanyika katika kijiji cha Malula kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwa tegemeo la hakika la malighafi itakayotumiwa kiwandani. Aidha kiwanda cha kutengeneza bidhaa zitokanazo na maziwa k.m bata, jibini n.k. kitaweza kunufaika kutokana na zao la maziwa kupatikana kwa wingi-mfano uzalishaji bidhaa hizo unafanyika katika kiwanda cha KCC nchini Kenya.
- Uzalishaji wa umeme katika mto Kikuletwa ambao unagawa ukanda wa uwekezaji na Wilaya ya Simanjiro una uwezo wa kuzalisha megawati 40 za umeme. Fursa hii ikitumika kwa manufaa, upo uwezekano wa kupunguza uhaba wa nishati hii kwa matumizi ya shughuli za kibiashara na uchumi zitakazoanzishwa.
- Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za mbogamboga zitakazozalishwa kwa kutumia maji ya mto Kikuletwa na zile zinazozalishwa kutoka Ngarenanyuki na kusafirishwa kupelekwa Siha na soko la Kilombero, Jijini Arusha zitakuwa malighafi itakayotumika katika kiwanda hiki.

## 3.9 UZALISHAJI WA KILIMO CHA NYANYA

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ina eneo linalolimwa zao la nyanya lenye hekta 1,460 kutokana na hali ya hewa inayofaa kwa zao hilo na upatikanaji wa mvua na maji ya umwagiliaji ambavyo vinachangia kustawi kwa zao hili. Zao hili linastawi na kulimwa kikanda kulingana na baadhi ya vigezo tajwa hapo juu.

Hata hivyo wakulima wa zao hili wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi zikiwemo kupata hasara wakati wa mavuno kwa kukosa soko na bei nzuri, na pia mazao mengi kuharibika kwa kuoza kutokana na kukosa vifaa bora vya kuhifadhia.

Kata inayolima zao hili kwa wingi ni Ngarenanyuki yenye wakazi 20,379 ambayo iko kwenye ukanda wa juu wenye hali hewa nzuri na uhakika wa mvua kwa mwaka mzima. Kwa sasa eneo la ekari 1,200 zinazotumika kwa kilimo cha nyanya ambapo mavuno ni wastani wa tani 120,000 kwa mwaka.

**Fursa zilizopo**

**Ujenzi wa kiwanda cha usindikaji wa nyanya**

Kama zilivyo bidhaa zote za mbogamboga, nyanya hazimudu kukaa kwa muda mrefu katika hali ya kawaida bila kuharibika.

Hivyo kuepuka hasara wanayopata wakulima tunaona ni vema kukajengwa kiwanda cha kusindika nyanya. Kiwanda hiki kitatumika kuhifadhi nyanya, kuzisindika na kuziweka kwenye vifungashio ambavyo vitafanya bidhaa hii kuongezeka thamani na kutumika kwa muda mrefu.

Kiwanda hiki kitakuwa soko la uhakika kwa wakulima wa maeneo hayo na hivyo kuwaongezea kipato.

## 3.10 MJI WA USA RIVER

Mji wa Usa River ni Makao Makuu ya Wilaya ya Arumeru, na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Mamlaka ya Mji mdogo wa Usa River ilianzishwa mwaka 2009 baada ya kutangazwa kupandishwa hadhi ya kuwa mamlaka ya mji mdogo kupitia tangazo la Serikali namba 153 la tarehe 17/09/ 2004. Kupitia sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, mji huu ulikuwa na jumla ya watu 18,000, kwa sasa unakadiriwa kuwa na jumla ya watu 23,437.

Huduma za kiuchumi na kijamii zipatikanazo ndani ya mji wa Usa River ni pamoja na Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Arumeru, Taasisi za fedha (Kama vile Benki ya Watu wa Meru, Tawi la Benki ya CRDB, Tawi la Benki ya NMB, na Tawi la Benki ya Posta), makao makuu ya Posta ya Wilaya, Ofisi ya kata ya Usa River, Vyuo vya Elimu ya Juu, Hoteli za Kitalii, n.k.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru tunalenga kuuendeleza
mji wa Usa River kama kituo mji wa kitalii na vyuo vya Elimu ya Juu, hii inatokana na ukweli kuwa eneo hili linaunganishwa vizuri sana na maeneo mengine yaliyopo ndani na nje ya Nchi kwa njia ya barabara na usafiri wa anga. Mji wa Usa River upo umbali wa kilometa zipatazo 20 kutoka jijini Arusha, unaunganishwa na Jiji la Arusha na Manispaa ya Moshi kwa barabara ya lami. Mji wa Usa River upo umbali wa kilometa 25 kutoka uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro.
Mji huu upo katika ukanda wa kaskazini wa kitalii na una hali nzuri sana ya hewa inayovutia watu mbali mbali kutoka ndani na nje ya Nchi kutaka kuishi/kufanya kazi kwenye eneo hili. Mwekezaji yeyote yule anayetaka kuwekeza kwenye eneo hili atapata fursa kubwa ya kiuchumi kutokana na kuwepo kwa mtandao wa kutosha wa miundo mbinu mingi ya msingi ya kiuchumi na kijamii. Pamoja na hayo yote pia kuna eneo la Kili Golf lenye viwanja vya michezo vyenye hadhi ya kimataifa, kuna uwanja mkubwa wa gofu wenye mashimo 18, na kiwanja cha mbio na michezo ya farasi. Michezo ya namna hiyo mara nyingi sana hupendwa na wageni hasa watokao nje ya Nchi.
Katika mji wa Usa River pia tuna fursa nzuri sana ya kuendesha shughuli za kitalii zinazozingatia kuhifadhi mazingira. Kilometa 5 kaskazini ya mji huu kuna msitu wa asili unaotumika kama makazi ya wanyamapori wachache kama vile mbega weupe na aina nyingi ya ndege.

Kwa upande wa vyuo vya Elimu ya Juu, Mji wa Usa River una idadi ya kutosha ya vyuo hivyo, Chuo Kikuu cha Meru, chuo kikuu cha Makumira, Chuo cha Maendeleo ya Jamii, na Taasisi ya Elimu ya Nelson Mandera, hivi ni vichache miongoni mwa vilivyopo. Pia kuna Taasisi nyingine za Elimu zinazotoa mafunzo Astashahada na Stashahada, Chuo cha Elimu Patandi, Chuo cha Mifugo Tengeru, Kituo cha Walemavu Usa River, na Kituo cha Taasisi ya mafunzo ya uongozi (Danish Centre), ni miongoni mwa baadhi ya vyuo hivyo. Kati ya vyuo vyote hivyo, Taasisi ya Nelson Mandela inatarajiwa kuvutia zaidi wawekezaji wengine kwenye tasnia hiyo kuwekeza katika mji wa Usa River.

Taasisi hiyo ina eneo lenye ukubwa wa ekari 3,285, kitakapofikia katika uwezo wake kamili wa uendeshaji kitachangia sana katika ukuaji wa mji huu kwa kuvutia wawekezaji wengine sio katika sekta ya Elimu ya Juu tu bali hata katika sekta nyingine za maendeleo ya kiuchumi na kijamii

Mji wa Usa River upo karibu sana na Hifadhi ya Taifa ya Arusha na mlima Meru. Ukiwa katika mji huu unaweza kuona vizuri paa la Afrika (Mlima wa Kilimanjaro) na mlima wa pili kwa urefu hapa Nchini (Mlima Meru). Hifadhi ya Taifa ya Arusha ni tajiri sana katika maliasili, kuna aina nyingi sana ya wanyama na mimea.

Ukiwa katika Hifadhi hiyo unaweza ukajipima uwezo wako wewe mwenyewe kwa kupanda mlima Meru unaoaminika kuwa mgumu zaidi kuupanda kuliko mlima Kilimanjaro. Kwa kuamua kupumzika katika mji wa Usa River unapata fursa ya kufurahia mazingira mazuri na hali nzuri ya hewa kabla ya kuanza kutembelea Hifadhi za Taifa zilizopo katika eneo hili la kaskazini mwa Nchi.

Ukiwa katika mji huu pia unaweza kujionea na kupiga makasia katika ziwa la ajabu la Duluti, ni ziwa pekee kwenye eneo hili ambalo maji yake hayatokani na mtiririko wa maji kutoka kwenye mito au chanzo kingine chochote cha maji.

## 3.11. MJI WA KIA

Mji wa KIA upo karibu sana na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, ni kiasi cha kilometa 6 tu kutoka uwanjani hapo pembezoni mwa barabara kuu ya Moshi – Arusha. Katika mji huu kuna mambo makuu matatu yanayosababisha na kuchangia katika ukuaji wa mji huu; mambo hayo ni uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, njia ya reli ya kutoka Arusha hadi Tanga na Dar es Salaam, na barabara ya lami kutoka Dar es Salaam hadi Arusha.

Sehemu ya eneo hili ilitangazwa kuiva kwa ajili ya kuendelezwa kimji mwaka 2010 na viwanja vipatavyo 3,814 vimepangwa na kuanza kupimwa. Karibu na eneo hili kuna maeneo makuu mawili ambayo ni muhimu sana katika shughuli za uwekezaji, maeneo hayo ni lile linalosimamiwa na Shirika la Uendelezaji la Uwanja wa Kimataifa wa ndege wa Kilimanjaro (KADCO), na eneo lenye ukubwa wa ekari 4,000 lililolengwaa kutumika kwa ajili ya shughuli za uwekezaji kiuchumi (Special Economic Zone).

Meneo yote hayo yanaweza kutumika kwa ajili ya kujenga maghala ya kuhifadhia bidhaa zinazozalishwa viwanda na hata maua na mboga mboga zinazosafirishwa nje ya Nchi kupitia uwanja wa ndege wa Kilimanjaro.

Kutokana na eneo hili kuunganishwa vizuri kwa njia ya reli na barabara ya lami na bandari za Tanga na Dar es Salaam, uwekezaji ya viwanda kwa ajili ya kuongezea thamani bidhaa malighafi zizalishwazo hapa Nchini unafaa zaidi kwa ajili ya bidhaa zizalishwazo katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha kabla ya kusafirishwa kwenda Ulaya, Marekani na maeneo mengine mbali mbali hapa Duniani. Eneo hili linaweza kutumika kama kituo kikuu cha viwanda kwa ajili ya kuongezea thamani bidhaa zizalishwazo katika kanda ya kaskazini.

Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro utakuwa ni jukwaa kuu kuunganisha kanda ya kaskazini na maeneo mengine hapa Duniani. Utaendelea kutumika kama mlango mkuu wa kuingilia na kutokea katika miji mbali mbali iliyopo katika kanda hii ya kaskazini, kusafirishia bidhaa mbali mbali kwenda nje ya Nchi, kuingiza watalii na wawekezaji mbali mbali wanaolenga kuwekeza kwenye eneo hili, yaani maeneo ya mikoa ya Kilimanjaro, Manyara na Arusha. Kutokana na eneo hili kuunganishwa vizuri na maeneo mengine ndani na nje ya Nchi kwa Barabara ya lami, reli na uwanja wa ndege wa Kimataifa, eneo hili linaendelea kuwa miongoni mwa maeneo mazuri kabisa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji kiuchumi.

## 3.12 UFUGAJI NYUKI

Halmashauri ya Meru ina jumla ya vikundi 35 vya wafugaji nyuki na wafugaji binafsi

570.

Ndani ya Halmashauri ya Meru kuna Jumla ya Mizinga ya nyuki 2,226 na takwimu za uvunaji zinaonyesha kuwa kwa mwaka asali ya nyuki wakubwa hufikia kilo 5,933 na asali ya nyuki wasiouma hufikia kilo 1,805. Mazao mengine ya asali yanayopatikana ni Pamoja na kilo 619 za Nta na Gundi kilo 15.

## 3.13 VIVUTIO VYA UTALII VINAVYOPATIKANA HALMASHAURI YA WILIYA YA MERU

| | KIVUTIO | MAHALI KILIPO | SHUGHULI ZA KITALII ZINAZOWEZA KUFANYIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Hifadhi yaTaifa - ANAPA | Meru | Kupanda Mlima Meru, wenye vilele vitatu; Uhuru, Sado na Tulululusia. Kuona vivutio mbalimbali ikiwemo Ziwa Momela makazi ya ndege aina ya Flamingo. Ngurdoto kreta, wanyama mbalimbali kama Tembo, Pundamilia, Twiga, Mbega Weupe, Nyani, nk |
| 2. | Msitu wa User-Spring (Kibola) | Nkoanenkoli | Upigaji picha, Mbega weupe na aina mbalimbali za miti ya asili na viumbe wadogo nyoka, tumbili, ndege wa msituni |
| 3. | Msitu wa Kalanga | Nkoanenkoli | Picha na kutembea ndani ya msitu mnene. |
| 4. | Msitu wa Naic | Nshupu | Picha na kutembea ndani ya msitu upatikanaji wa wanyama jamii ya kima na ndege wa msituni. |
| 5. | Mlima Sakila | Sakila | Upandaji mlima. |
| 6. | Maporomoko ya maji | Ulon'ga | Kutazama maanguko ya maji. |
| 7. | Mapango ya mlima Shumbumbu | Akheri | Mapango yaliyotumika kama maandaki wakati wa vita wa vya Wameru na wa Masai. |
| 8. | Ziwa duluti (lake duluti) | Akheri | Mvuvi wa kitalii , upigaji picha na kutembea ndani ya msitu |
| 9. | Mringaringa | Poli | Utalii wa utamaduni – vinyago, ngoma za asili, shughuli za ibada, matambiko, burudani, vipo vikundi kadhaa vya burudani kama vile; Kikundi cha utamaduni cha Mulala, Tengeru |